

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI IFAKARA



Unapojibu tafadhali taja:

Toleo. Na. 2

TAARIFA KWA UMMA

YAH: TAHADHARI DHIDI YA UGONJWA WA HOMA YA TUMBO

Ifakara, Morogoro Tarehe 12/12/2024

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara **Bi. Zahara Michuzi** anawatangazia Wananchi wote wa Halmashauri ya Mji Ifakara kuwa kumekuwepo na ongezeko la Ugonjwa wa Homa ya Tumbo katika Halmashauri ya Mji Ifakara kutohana na mabadiliko ya hali ya Hewa katika kipindi hiki cha Mvua. Hivyo basi ili tuweze kujikinga Wananchi wote tunatakiwa kufanya mambo yafuatayo; -

- ✓ Kufanya Usafi unaoridhisha na kudhibiti utiririshaji wa majitaka kwenye Maeneo yetu ya Makazi, biashara na huduma.
- ✓ Kunywa maji safi na Salama kwa kuyachemsha au kuyatibu kwa kutumia dawa maalumu ya kutibu maji, kuchujwa na kutunzwa katika chombo kisafi.
- ✓ Tumia choo bora kujisaidia na kuzingatia usafi wa choo baada ya kukitumia ikiwemo kufunikwa tundu la choo ili kuzuia nzi na mende.
- ✓ Epuka kujisaidia nje ya Choo ikiwemo vichakani.
- ✓ Kuondoa taka zote zilizorundikwa kwenye maeneo ya makazi, biashara, soko na huduma.
- ✓ Zingatia njia sahihi za usafi wa chakula ikiwemo kula chakula kikiwa chamoto.
- ✓ Kuosha Matunda na mbogamboga kwa Maji tiririka kabla ya kula
- ✓ Kunawa Mikono kwa maji tiririka na sabuni.
- ✓ Kuepuka kunywa juisi zilizoandaliwa kienyeji mtaani.

Upatapo Tangazo hili, Tafadhali mjulishe na mwingine.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Halmashauri ya Mji Ifakara

